**BENKI KUU YA TANZANIA**
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
**TANZANIA**
Simu: +255 22 223 3167
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz

**BANK OF TANZANIA**
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
**TANZANIA**
Phone: +255 22 223 3167
Email: botcommunications@bot.go.tz

23 Machi 2024

## TAARIFA KWA UMMA

## BENKI KUU YA TANZANIA KUENDELEZA JUHUDI ZA KUKABILIANA NA UPUNGUFU WA FEDHA ZA KIGENI

Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika Soko la Jumla la Fedha za Kigeni, kwa kuuza dola ya Marekani kwa benki za biashara ikiwa ni sehemu ya juhudi zinazoendelea za kupunguza uhaba wa fedha za kigeni nchini.

Mpango huu unalenga kuhakikisha kuna ukwasi wa kutosha wa fedha za kigeni katika soko. Vilevile, mpango huu unalenga kuhakikisha kuwa wananchi wenye uhitaji halali wa ya fedha za kigeni wanapata huduma hiyo kwa bei ya soko kupitia Taasisi rasmi za fedha nchini.

Ni muhimu kwa wadau wote kuelewa kuwa ushiriki wa Benki Kuu ya Tanzania katika Soko la Jumla la Fedha za Kigeni unazingatia Sera ya Ushiriki katika Soko la Fedha za Kigeni (Foreign Exchange Intervention Policy) yenye lengo la kukuza utulivu wa soko na kukidhi mahitaji halali ya fedha za kigeni nchini.

Idara ya Mawasiliano
**BENKI KUU YA TANZANIA**